



WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI



(RITA)

TAARIFA KWA UMMA

KUKANUSHA TAARIFA ZA UPOTOSHAJI KUHUSU ZOEZI LA UHAKIKI WA VYETI VYA KUZALIWA KWA WANAFUNZI WANA OOMBA MIKOPO YA MASOMO YA ELIMU YA JUU.

RITA inapenda kuutaarifu Umma kwamba kuna taarifa inasambazwa katika mitandao ya kijamii ikitoa taarifa potofu kuhusu zoezi linaloendelea la uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na vifo kwa wanafunzi wanaoomba mikopo ya masomo ya elimu ya juu kwa mwaka 2017/2018.

Taarifa hiyo inaeleza kwamba, kwa wanafunzi waliopata vyeti vya kuzaliwa kuanzia mwaka 2010 na miaka kabla ya hapo (akiviita vyeti virefu) taarifa za vyeti hivyo hazipo katika mfumo wa kompyuta hivyo wakifika kuhakiki watalazimika kuomba upya cheti cha kuzaliwa ikiwa ni pamoja na kulipa ada ya TShs. 30,000.

Wakala unakanusha taarifa hizo kwamba sio za kweli hivyo tunawaomba wananchi wazipuuze. Ukweli ni kwamba vyeti vyote vilivyotolewa katika Ofisi za Wakala Tanzania Bara bila kujali ukumbwa na umbo lake ni vyeti halali na wananchi wanaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata huduma nyingine na taarifa zote za waliosajiliwa zipo na zimehifadhiwa sehemu salama tayari kutumika mara zinapohitajika.

Ifahamike kwamba kuhakiki vyeti vya kuzaliwa vya wanafunzi sio utaratibu mpya ambapo kwa miaka ya nyuma vyeti vilikuwa vinaletwa RITA na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu baada ya wanafunzi kutuma maombi ya Mkopo lakini hivi sasa umeboreshwa na wanafunzi wanahakiki vyeti vyao kabla ya kutuma maombi utaratibu ambao unampa nafasi ya kuomba cheti cha kuzaliwa mara inapobainika kwamba cheti alichokuwa nacho si halali hivyo kumuwezesha kuendelea na utaratibu wa kuomba Mkopo. Kwa mfano, katika uhakiki wa mwaka 2016/17 zaidi ya vyeti 500 vya wanafunzi vilibainika kuwa ni vya kughushi

Tunatoa rai kwa wanafunzi kuendelea kuhakiki vyeti kwa njia tatu zilizopo ambazo ni;

- Kuhakiki vyeti vyake katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya alipokipata cheti hicho
- Kwa njia ya Mtandao kwa wanafunzi wanaoishi Wilaya ambayo sio walikopata cheti ambapo watatakiwa kutuma nakala ya vyeti vyake pamoja na risiti ya malipo ya ada ya uhakiki kupitia barua pepe uhakiki@rita.go.tz
- Kufika katika Ofisi za Makao Makuu ya Wakala zilizopo katika Jengo la RITA Tower Mtaa wa Makunganya na Simu Mkabala na ilipokuwa Club Billicanas, Jijini Dar es Salaam.

- *Kumbuka:* Ada ya Uhakiki kwa njia yoyote kati ya zilizotajwa hapo juu ni TShs. 3,000 kwa kila cheti na zilipwe katika Benki ya NMB kwenye akaunti ya

Administrator General Collection Account namba 20610009881.

Tunachukua fursa hii kuwaonya wale wote wanaosambaza taarifa potofu kwa wananchi kuhusu Wakala na Huduma inazotoa na yoyote atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria husika.

Taarifa na Maelezo zaidi zinapatikana katika tovuti yetu www.rita.go.tz , ukurasa wetu wa [facebook.com/ritatanzania](https://www.facebook.com/ritatanzania) au simu namba 0719 593 179.

Emmy Kalomba Hudson
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu – RITA

17 Agosti 2017